



Simu: +255 26 2322761-5
Fax No. +255 26 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz

BUNGE LA TANZANIA

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S. L. P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge vitaanza tarehe **5 hadi 25 Oktoba, 2026 jijini Dodoma**. Vikao hivyo vinafanyika kabla ya **Mkutano wa Tano wa Bunge** utakaoanza tarehe **27 Oktoba, 2026**.

Katika kipindi hicho, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (**PAC**), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (**LAAC**), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (**PIC**) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti zitatangulia kuanza vikao tarehe **5 Oktoba, 2026**.

Kamati kumi na moja (11) zilizosalia zitaanza vikao tarehe **12 Oktoba, 2026**. Shughuli zilizo-pangwa katika Kamati zote ni zifuatazo: -

1.0 Kuchambua Sheria Ndogo

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo itafanya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nne wa Bunge.

2.0 Kupokea na Kujadili Taarifa Mbalimbali za Utendaji wa Serikali na Taasisi zake

Kamati kumi na moja za kisekta zitapokea na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji wa Serikali na Taasisi zake.

Aidha, Kamati ya Bajeti itapokea na kujadili taarifa mbalimbali kutoka Serikalini kwa lengo la kutekeleza jukumu lake la kusimamia, kuchambua, kuratibu na kulishauri Bunge kuhusu sera za fedha za umma, mapato ya Serikali, Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

3.0 Kuchambua Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kamati ya PAC na LAAC, zitachambua Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu hesabu zilizokaguliwa za wizara, taasisi, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2025.

1/2



[bungetz1](#) | [bunge_tz](#) | [bunge.tanzania](#) | Bunge TV | [www.parliament.go.tz](#)

4.0 Kupokea na kuchambua Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Kamati ya PIC itapokea na kuchambua Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na miongozo mujarabu ya biashara.

5.0 Kupokea na Kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti itapokea na kujadili Mapendekezo ya Mpango una-okusudiwa kutekelezwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha 2027/2028 ili kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kuhusu Mwongozo wa kuandaa Bajeti ya Serikali, vyanzo vya mapato ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Serikali na vipaumbele kuhusu Mpango huo.

Ratiba ya vikao vya Kamati zote inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni **[www.bunge.go.tz](#)**.

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,
Ofisi ya Bunge,
DODOMA.

01 Oktoba, 2026.